

Darasa la Majaribio la Misingi ya utetezi wa Kijamii katika Utawala wa Sekta ya Madini, Mafuta na Gesi

HakiRasilimali na MS TCDC (waandaaji) wameunda kozi ambayo itasababisha uwezo wa jamii za wenyehi kushinikiza ajenda za utetezi zinazoongozwa na mahitaji, na hivyo kuathiri Sera na Miongozo ya kisekta.

Timu ya wataalam ilihusika katika uandaaji wa mtaala wa masomo na moduli, ambazo baadaye zilithibitishwa na wadau muhimu na wakufunzi. Tunafurahi kutangaza kuwa programu itaanza tarehe 21 Septemba hadi 2 Oktoba 2020 huko MS TCDC, Arusha kwa kuwa na darasa la kwanza la majaribio.

Moduli za kozi hii ni; *Misingi ya sekta ya Uziduaji; Utawala wa sekta ya uziduaji; Usimamizi wa mapato ya sekta ya uziduaji; Uchimbaji na Maendeleo ya Mitaa; Haki za Binadamu na athari za kimazingira katika sekta ya uziduaji; Uwazi, Uwajibikaji, na Uadilifu katika sekta ya uziduaji; uchimbaji mdogo; Jinsia na masuala mengine mtambuka; Utetezi wa sera inayoongozwa na jamii; Mbinu ya mawasiliano na usambazaji wa taarifa.*

Mafunzo haya yatafanyika kwa wiki mbili (2) mfululizo. Ili kuhakikisha ubora, uendelevu, na umuhimu, waandaaji wanaamini kwamba darasa hili la majaribio halitatumika tu kujaribu moduli na mbinu inayopendekezwa kwa jumla lakini pia kuhakikisha usawa/mlinganyo kati ya mahitaji ya jamii na utetezi.

Wataalam na wabobezi wa sekta watatumika kuwa wawezeshaji wa moduli. Pia, wakufunzi hawa watapata fursa ya kusikia kutoka kwa wageni mbalimbali walioalikwa kutoa uzoefu wao katika utetezi kutoka kwenye sekta za madini, mafuta, na gesi asilia.

Registration No. 00NGO/R2/00074

Board of Directors: Chairperson: - Donald Kasongi – Governance Links • Vice Chairperson: - Semkae Kilonzo-Policy Forum • Members • Alphonse Gura-Tanganyika Law Society, Flaviana Charles –Business and Human Rights Tanzania, Dr. Rugemeleza Nshala- Lawyers Environmental Action of Tanzania, Nicomedes Kajungu- National Union of Mining and Energy Workers, Jimmy Luhende-Action for Democracy and Local Government • Secretary: - Racheal Chagonja